

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA MTWARA (“Mtwara WSSA”) KWA MWAKA 2017/18 – 2019/20

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-17-014

Mnamo tarehe 18 Disemba 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Mtwara (Mtwara WSSA) la kutaka kurekebisha bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina ya Mteja	Matumizi (Mita za Ujazo)	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
		2016/17	%	2017/18	%	2018/19	%	2019/20
			Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	0-10	945	16%	1,100	9%	1,200	8%	1,300
	>10-20	1,090	10%	1,200	8%	1,300	8%	1,400
	>20	1,190	9%	1,300	4%	1,350	7%	1,450
Taasisi	0-11	1,735	44%	2,500	4%	2,600	4%	2,700
	>10-20	1,835	42%	2,600	6%	2,750	4%	2,850
	>20	2,030	31%	2,650	6%	2,800	4%	2,900
Biashara	0-10	1,735	44%	2,500	4%	2,600	4%	2,700
	>10-20	1,885	38%	2,600	4%	2,700	4%	2,800
	>20	2,080	30%	2,700	2%	2,750	4%	2,850
Viwanda	0-10	1,735	44%	2,500	4%	2,600	4%	2,700
	>10-20	1,885	38%	2,600	4%	2,700	4%	2,800
	>20	2,080	30%	2,700	4%	2,800	4%	2,900

Magati	Mita za Ujazo	1,000	50%	1,500	0%	1,500	0%	1,500
Wateja wa Maboza	Mita za Ujazo	3,000	17%	3,500	3%	3,600	0%	3,600

Jedwali 2: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Aina za Wateja	Bei za Sasa	Bei zinazopendekezwa					
	2016/17	% Badiliko	2017/18	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20
Majumbani	20,000	25%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Taasisi	30,000	33%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Biashara	30,000	33%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Viwandani	40,000	25%	50,000	0%	50,000	0%	50,000

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Customer Category	Bei za Sasa		Bei zinazopendekezwa				
	2016/17	% Badiliko	2017/18	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20
Majumbani	20% ya gharama za vifaa vya maunganisho	25%	25% ya gharama za vifaa vya maunganisho				
Taasisi							
Biashara							
Viwandani							

Jedwali 4: Tozo za Huduma za Sasa na zilizopendekezwa (Shilingi/mwezi)

Aina za Wateja	Bei za sasa		Tozo zilizopendekezwa kwa miaka mitatu		
	2016/17	% Badiliko	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	2,000	-100%	0	0	0
Taasisi	5,000	-100%	0	0	0
Biashara	5,000	-100%	0	0	0
Viwandani	6,000	-100%	0	0	0

Kutokana na wasilisho la Mtwara WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji, kupata fedha kuongeza uwekezaji ili kupanua huduma zake, kulinda vyanzo vya maji vya Mtawanya na Mchuchuma pamoja na kupanua mtandao wa usambazaji maji kutoka kilomita 221 za sasa.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 27 Septemba, 2018, katika ukumbi wa VETA, Mtwara Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **08 Oktoba, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA EWURA, KANDA YA MASHARIKI, GHOROFA YA SABA, JENGO LA LAPF, MAKUMBUSHO, DAR ES SALAAM** au ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Mtwara zilizopo Barabara ya Dar es Salaam/Mtwara, Mkabala na Shule ya Sekondari Mtwara.

**Imetolewa na
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**